

**Tarehe 5 Machi 2024:** Uchaguzi wa Kila Mwaka wa Jiji na Uchaguzi wa Uteuzi wa Wagombea Urais

**TAFADHALI KUMBUKA: Kutakuwa na kura mbili tofauti mnamo mwezi Machi.**

- Karatasi za kura ya Uchaguzi wa Kila Mwaka wa Jiji zitatumwa **kwa wapiga kura wote walioandikishwa na wanaostahili.**
- Karatasi za kura ya Uteuzi wa Wagombea Urais zitatumwa **kwa wapiga kura walioagiza pekee.**

**Kupiga Kura Mapema**

- **KURA ZA UCHAGUZI WA KILA MWAKA WA JIJI** zitatumwa kwa wapiga kura wote walioandikishwa na wanaostahili katika Burlington kufikia tarehe 14 Februari. Ikiwa hutapokea karatasi yako ya kura kufikia tarehe 21 Februari, tafadhali wasiliana na Ofisi ya Karani/Mweka Hazina.
- **Makaratasi ya kura za UTEUZI WA WAGOMBEA URAIS HAZITATUMWA** kwa wapiga kura wote. Ikiwa ungependa kuomba utumiwe makaratasi haya ya kura, tafadhali omba mtandaoni katika [mvp.vermont.gov](http://mvp.vermont.gov) au upigie ofisi ya Karani wa Jiji kupitia (802) 865-7000.
- Fuata maelekezo yote kwa umakini unapojaza kura yako ya barua. Hakikisha UMESAINI bahasha na UMEFUNGA karatasi ya kura yako ndani au kura yako haitahesabiwa.
- Rudisha karatasi ya kura uliyopiga:
  - **Kwenye jumba la City Hall kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa, saa 8:00 asubuhi hadi 4:30 jioni.**
    - Jumatatu hadi Ijumaa, saa 8:00 asubuhi hadi 4:30 jioni hadi kufikia tarehe 1 Machi.
    - Mnamo Jumatatu, Machi 4, kuanzia saa 8:00 asubuhi hadi 1:00 mchana.
  - **Kwenye Kisanduku cha Kuweka Kura kinachopatikana kwenye:**
    - Ukumbi wa jiji – upande wa Barabara Kuu wa jengo toka Ukumbi wa Michezo wa Flynn
    - Idara ya Kazi za Umma – 645 Pine Street
    - Kituo cha Zima Moto #2 – 132 North Avenue, nyuma ya jengo
    - Robert Miller Community Center – 130 Gosse Court
    - Kituo cha Zima Moto #3 – 20 Mansfield Avenue
  - **Kwenye kituo chako cha kupigia kura Siku ya Uchaguzi kati ya saa 7:00 subuhi na 7:00 jioni.** Orodha ya vituo vya kupigia kura inaweza kupatikana katika <https://www.burlingtonvt.gov/CT/Maps-Wards-State-Districts-and-Polling-Places>
    - **Kutokana na vikwazo vya jiji, wadi na eneo lako la kupigia kura zinaweza kuwa zimebadilika.** Thibitisha wadi unayoishi katika <https://www2.burlingtonvt.gov/Clerk/Elections/Map/>

**Kura ya Kujipeleka Moja kwa Moja**

- Maeneo ya kupigia kura yatafunguliwa kuanzia saa 7:00 asubuhi na 7:00 jioni katika Siku ya Uchaguzi
- Kuja pamoja na karatasi ya kupiga kura uliyotumiwa kwenye eneo lako la kupigia kura. Ikiwa hukupoea karatasi ya kupiga kura au hukuja nayo, bado utaweza kupiga kura. Hata hivyo, utaombwa usaini hati ya kiapo kwanza.
- Wapiga kura watakaoshindwa kufika kwenye eneo la kupigia kura, kutokana na ugonjwa au ulemavu, wanaweza kuwasiliana na ofisi ya Karani na kuomba kupiga kura kando ya barabara katika eneo la kupigia kura, kutuma karatasi za kupigia kura kwa njia ya kielektroniki, au kupelekewa karatasi za kura nyumbani na mjumbe wa Justices of the Peace.

### **Tarehe Muhimu**

**Tarehe 14 Februari** – Karatasi za kura za Uchaguzi wa Kila Mwaka wa Jiji zitatumwa kwa wapiga kura wote walioandikishwa

**Tarehe 4 Machi, saa 1 mchana** – Siku ya mwisho ya kujiandikisha kupiga kura mtandaoni au kwenye Ofisi ya Karani Mweka Hazina kabla ya Siku ya Uchaguzi; Unaweza kujiandikisha katika Siku ya Uchaguzi katika eneo lako la kupigia kura tarehe 5 Machi.

**Tarehe 4 Machi, saa 4:30 jioni.** – Siku ya mwisho ya kupeleka karatasi ya kura uliyopiga kwenye kisanduku cha kuweka kura

**Tarehe 5 Machi** – Siku ya Uchaguzi! Vituo vya Kupigia Kura vitafunguliwa saa 7:00 asubuhi hadi 7:00 jioni.

### **Ufikiaji wa Huduma za Lugha**

- Ikiwa unahitaji mkalimani Siku ya Uchaguzi, au wakati wa kura za mapema, tafadhali muulize mfanyakazi katika ofisi ya Karani au afisa wa uchaguzi katika eneo lako la kupigia kura. Una haki ya kupata mkalimani BILA MALIPO. Ofisi ya Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi (CEDO, Community & Economic Development Office) ya Jiji la Burlington, hutoa huduma za ukalimani kwa zaidi ya lugha 240.